



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
HALMASHAURI YA WILAYA YA TUNDURU



MKOA WA RUVUMA
Simu Na. +255 (026) 80004
Nukushi Na. +255 (026) 80208
Barua Pepe: info@tundurudc.go.tz.

Mtaa wa Kalanje
S.L.P 275
TUNDURU,

Unapojibu tafadhali taja

Kumb. Na. TDC/L.40/21/VOL.II/89

Tarehe 21/07/2020

TANGAZO LA NAFASI ZA KAZI.

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Tunduru anapenda kuwatangazia waombaji wenye sifa za kazi Mbalimbali waweze kutuma maombi kama zifuatazo:-

**1.MSAIDIZI WA KUMBUKUMBU II (RECORDS MANAGEMENT ASSISTANT II)
NAFASI MOJA (01)**

(a)Sifa za muombaji;-

(i) Wenye elimu ya kidato cha nne/Sita wenye cheti cha utunzaji wa kumbukumbu katika moja wapo ya fani za Afya,Masjala,Mahakama na Ardhi.

(b)Kazi/ Majukumu ya Kufanya:-

- (i) Kutafuta kumbukumbu/nyaraka/Mafaili yanayo hitajiwa na Wasomaji
- (ii) Kudhibiti upokeaji/Uandikishaji wa kumbukumbu au Nyaraka
- (iii) Kuchambua/Kuorodhesha na kupanga Kumbukumbu/Nyaraka katika makundi kulingana na somo husika kwa ajiri ya matumizi ya ofisi.
- (iv) Kuweka/Kupanga kumbukumbu/Nyaraka katika reki(File racks/Cabinets) katika masjala/vyumba vya kuhifadhia kumbukumbu.
- (v) Kuweka kumbukumbu (barua,Nyaraka n.k)katika mafaili.
- (vi) Kushughulikia maombi ya kumbukumbu/Nyaraka kutoka Taasisi za Serikali.

MSHAHARA:-Ngazi ya Mshahara wa Serikali yaani TGS B

2.MHUDUMU WA JIKONI II.NAFASI MOJA (01)

(a) Sifa za Muombaji:

(i)Wenye elimu ya kidato cha nne walio na uzoefu wa kazi kwa muda usiopungua miaka mitatu(3).

(b)Kazi na majukumu:-

- (i) Kusafisha vyombo vya kupikia
- (ii) Kusafisha vyombo vya kulia chakula
- (ii) Kuwatayarishia wapishi/Waandazi vifaa vya mapishi na Mezani
- (iv) Kusafisha maeneo ya kulia chakula na kupikia.
- (v) Kuwasaidia Waandazi na Wapishi.

MSHAHARA:-

Ngazi ya Mshahara wa Serikali yaani **TGOS A1**

MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA KWA WAOMBAJI WOTE;

- (i) Awe raia wa Tanzania mwenye umri kuanzia miaka 18 hadi 45
- (ii) Waombaji wanatakiwa kuwasilisha wasifu binafsi (CV) ikionesha mawasiliano ya wahusika, namba za simu na wadhamini watatu
- (iii) Waombaji wote lazima waambatanishe nakala ya vyeti vifuatavyo:-
 - (a)Astashahada/ cheti cha utaalum kulingana na sifa za kazi husika
 - (b)Cheti cha kidato cha nne au cha sita
 - (c)Cheti cha kuzaliwa
 - (d)Picha moja ya **PASSPORT SIZE** ya hivi karibuni.
 - (e)**Result slip au provisional results au transcript** hazitafanyiwa kazi
- (iv) Waombaji wenye vyeti vya kidato cha nne, cha sita na cheti cha Taaluma kutoka nje ya nchi wahakikishe vimehakikiwa na Baraza La Mititani La Taifa (**NECTA**) Na Baraza La Elimu Ya Ufundi La Taifa (**NACTE**)
- (v) Barua za maombi ziandikwe kwa kiswahili au kwa kiingereza
- (vi) Watakao chaguliwa kufanya usaili watajulishwa tarehe ya usaili
- (vii) Kwa waombaji wa nafasi ya Msaidizi wa Kumbukumbu Daraja la II ,cheti kinachopokelewa ni (**Technician Certificate NTA level 5**).
- (viii) Maombi yasiyozingatia vigezo vilivyoanishwa hayatafanyiwa kazi.
- (ix) Maombi yote yatumwe kwa njia ya Posta, maombi yatakayoletwa kwa njia ya mkono hayatapokelewa.

Mwisho wa kupokea maombi ni tarehe 04/08/2020 saa tisa na nusu (9:30) alasiri

Maombi yatumwe Kwa :-

Mkurugenzi Mtendaji,
Halmashauri ya Wilaya ya Tunduru,
S.L.P. 275,
TUNDURU


Gasper .Z. Balyomi
MKURUGENZI MTENDAJI(W)
TUNDURU.

MKURUGENZI MTENDAJI WILAYA
TUNDURU